BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Tano – Tarehe 05 Disemba, 2023.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Ikulu:

59. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

    Kwa kipindi cha miaka mitatu ya hivi karibuni, wanadiaspora wangapi mashuhuri wametembelea Zanzibar na kuonesha dhamira ya kuwekeza katika vitega uchumi au kuzitangaza fursa za uwekezaji kwenye sekta za utalii na biashara.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

33. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ujenzi wa soko la kisasa la Mwanakwerekwe ni jitihada kubwa za mageuzi ya kiuchumi zinazofanywa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi.

(a) Je, ni fursa gani ambazo wananchi wa jimbo la Mwanakwerekwe watanufaika na ujenzi wa soko hili jipya na la kisasa.

(b) Kwa kiasi gani watu wenye mahitaji maalum wamezingatiwa kuwa ni miongoni mwa wanufaika watarajiwa baada ya kukamilika kwa ujenzi wa soko hili hususan katika suala zima la uwepo wa miundombinu rafiki.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

39. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Mwinyi kwa uamuzi thabiti wa kutenga eneo maalum kwa ajili ya uwekezaji kwenye sekta za viwanda (Industrial Park) liliopo Chamanangwe Pemba)

(a) Je, ni wawekezaji wangapi mpaka sasa wa ndani na wa nje wameonesha nia ya kuwekeza katika eneo hilo.

(b) Ni kwa kiasi gani miundo mbinu ya uwekezaji katika eneo hilo imezingatia vyema suala la uhifadhi wa mazingira hususan uchafuzi wa hali ya hewa (Air pollution) utakaotokana na moshi mwingi wa viwandani.

(c) Ni kwa kiasi gani eneo limewekwa miundombinu ya kiusalama ili kuweza kuvutia zaidi wawekezaji makini (Seriously Investors).

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

61. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

    Tangu kuja mwandishi nguli wa riwaya duniani Abrazak Gurna hivi karibuni hapa nchini kwetu na kupokelewa kwa heshima kubwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

    (a) Ni mikakati gani mwandishi huyo aliiahidi kuitekeleza kwa pamoja katika kuinua kiwango cha uandishi wa vitabu na kukitangaza vyema kiswahili sanifu duniani.

    (b) Je, Wizara yako inampa mashirikiano gani mwandishi huyo katika kuhakikisha kwamba tasnia yake inaleta matokeo chanya katika makuzi ya lugha yetu adhimu ya kiswahili kwa ujumla wake.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

1. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

    Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuanzisha Wizara yako kwa lengo kubwa la kuwasaidia wananchi walio na kipato cha chini na wavuvi wadodo wadogo hasa wa vijijini. Katika kuwasaidia huko, Serikali ilikuja na mpango mzuri wa kuwakopesha boti pamoja na vifaa vyake kamili wavuvi wadogo wadogo, mpango ambao pamoja na mafanikio yake, unakabiliwa na changamoto mbali mbali.

    (a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuwakopesha boti wavuvi ambao hawamudu kuunda vikundi vya ushirika.

    (b) Je, Serikali haioni haja ya kuregeza masharti ili wavuvi wetu waweze kuimudu mikopo hiyo.

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

29. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Ni miji ama mitaa gani ambayo imekosewa katika suala zima la mipango miji na upi mkakati wa Serikali wa kuwa na mipango miji bora na ya kisasa itakayozingatia miundombinu bora na ya uhakika.

Wizara ya Afya:

19. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kutokana na idadi kubwa ya watu iliyoongezeka katika jimbo la Konde hasa baada ya matokeo ya sensa ya mwaka 2022, na takriban wakaazi wote hao wanatumia kituo cha afya cha Konde cha daraja la II.

(a) Je, ni lini Wizara itakifanya kituo hicho kuwa “Cottage” ili kuwasaidia wakaazi wa eneo hilo.

(b) Kwa kuwa idadi ya akina mama wanaojifungua katika kituo hicho ni kubwa na sehemu ya kujifungulia (maternity) ni ndogo na ina vitanda viwili tu. Je, Wizara ina mpango wowote wa kuongeza jengo la kujifungulia.

84. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Katika hospitali kuu ya Mnazi Mmoja kumejitokeza tabia kwa wahudumu wa afya “Orderly” wanaoajiriwa kutofanya kazi zao kama mikataba yao ya kazi inavyoelekeza.

(a) Je, Wizara yako inalifahamu vipi suala hili.

(b) Je, ni sababu zipi zinazopelekea kwa wahudumu wa afya hao kufanya kazi kinyume na mikataba yao inavyowaelekeza.

86. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Katika Hospitali zetu za Serikali kuna baadhi ya madaktari wanashindwa kutumia lugha nzuri kwa wagonjwa wakati wa kupokea vipimo vya maradhi yao hasa, pale vipimo hivyo vinapoonesha kuwa wagonjwa hao wana matatizo mbali mbali ya kiafya.

(a) Ni mbinu gani ambazo madaktari wanapaswa kuzitumia katika kumpatia mgonjwa majibu ya vipimo vinavyoonesha kuwa na tatizo.

(b) Ni adhabu gani za kisheria ambazo wanapaswa kupatiwa madaktari wanaokutwa na kadhia ya kutumia lugha mbaya kwa wagonjwa, hasa wanapopokea majibu ya vipimo vya matatizo yao.

<u>**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**</u>

65. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Historia inaeleza juu ya uwepo wa kaburi la juu kwa juu.

(a) Je, ni katika maeneo gani ya mji wa Zanzibar linapatikana kaburi hilo.

(b) Je, ni kwa kiasi gani kaburi hilo linaendelea kuhifadhiwa na ni nani aliyezikwa hapo na kwa nini alizikwa kwa utaratibu huo.

<u>**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**</u>

76. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Zao la muhogo limekuwa ni bidhaa muhimu kitaifa na kimataifa.

Je, ni zipi jitihada za Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda katika kuona kwamba wakulima wa zao la muhogo wananufaika na fursa mbali mbali za masoko ndani na nje ya nchi.

III. **HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa mara ya Pili.

**Zanzibar,**
**05 Disemba, 2023.**

**Raya Issa Msellem**
**KATIBU WA BARAZA.**